



Youth Allowance for job seekers

Youth Allowance for job seekers inakupa usaidizi wa kipesa kama una umri wa miaka 21 au mdogo zaidi na ukitafuta kazi, au huwezi kufanya kazi kwa muda.

Ustahiki wa Youth Allowance for job seekers

Sheria unazohitaji kuridhi ili kupata Youth Allowance for job seekers zinategemea hali yako.

Lazima uwe na umri wa kati ya miaka 16 na 21 na uridhe zote zifuatazo:

- sheria za ukaazi
- tathmini ya mapato.

Unahitajika pia kuwa mmojawapo ifuatayo:

- huna kazi na unatafuta kazi
- unaumwa au kujeruhiwa na huwezi kufanya kazi yako au somo ya kawaida kwa muda mfupi.

Huenda hutastahiki ikiwa unapata malipo fulani kutoka Department of Veterans' Affairs (DVA).

Hali yako ya sasa itaangaliwa ili kutathmini ustahiki wako wa Youth Allowance.

Viwango vya malipo kwa Youth Allowance for job seekers

Kiasi unachopata unaweza kubadilisha kulingana na hali yako ya kibinafsi. Hii ni pamoja na:

- kama una mpenzi
- kama una watoto
- kama ukiishi kwa nyumba ya wazazi wako
- kama ukiishi mbali ya nyumba ya wazazi wako ili kusoma, kupata mafunzo au kutafuta kazi
- ikiwa unamiliki rasilimali yoyote, kwa mfano mali isiyohamishika, hisa au uwekezaji unaosimamiwa
- kiasi gani cha mapato wewe na mpenzi wako mmepata katika siku 14 zilizopita.

Ikiwa unapata mapato zaidi ya kiasi fulani, yanaweza kuathiri kiasi gani unachoweza kupata.

Jinsi ya kudai Youth Allowance for job seekers

Unaweza kudai mtandaoni Youth Allowance for job seekers kwa kutumia akaunti yako mtandaoni ya Centrelink kupitia myGov. Ikiwa huna akaunti ya myGov au akaunti mtandaoni ya Centrelink, unahitajika kuanzisha hizi.

Kama unahitaji usaidizi kuanzisha akaunti yako ya mtandaoni, unaweza kuzungumza na wafanyakazi wetu. Tujulishe ikiwa unahitaji mkalimani, na tutapanga mmoja kwa bure.

Unaweza kuanza dai lako hadi ya wiki 13 kabla hali yako itakapobadilisha.

Inaweza kuwa kwa mojawapo ya sababu zifuatazo:

- unaacha masomo ya wakati wote
- utakuwa unafanya kazi saa chini zaidi na unakidhi tathmini ya mapato ya kibinafsi
- unajua kwamba utapoteza kazi yako.

Unaweza kuondoa dai lako wakati wowote ikiwa hali yako ya kipesa inabadilika.

Wakati utakapopata malipo yako ya kwanza

Utahitaji kukamilisha kazi zako za mwanzoni na kuripoti mapato yako kabla tunapoweza kutoa malipo yako ya kwanza.

Mara nyingi, utapata malipo yako ya kwanza ya Youth Allowance karibu wiki 2 baada ya sisi kuidhinisha dai lako. Huenda utahitaji kungoja muda zaidi ikiwa vipindi vyovyote vya kungojea vitatumika. Mara tu malipo yako yanaanza, tutakulipia kila baada ya wiki 2.

Tutakuambia ikiwa una kipindi cha kungoja na muda gani ambao utahitaji kungoja. Pia utahitaji kuripoti mapato yako pamoja na ya mpenzi wako kila baada ya wiki 2.

Tunahesabu vipindi vya kungojea vinavyotumika kwako tunapotathmini dai lako. Unaweza kutarajia kusikia kutoka kwetu ndani ya siku 21 ya kuwasilisha dai lako.

Muda unaotuchukua kutathmini dai lako hauathiri muda wako wa kungojea.

Mabadiliko ya hali

Unahitaji kutuambia kuhusu mabadiliko ya hali ndani za siku 14. Hii inajumuisha mabadiliko kwa yako:

- wazazi au walezi
- mpenzi
- watoto wanaotegemea.

Mabadilisho yanaweza kujumuisha:

- habari yako ya kibinafsi na ya mawasiliano
- mabadilisho ya masomo
- hali yako ya kuishi
- mabadilisho ya jina
- hali ya familia
- hali yako ya uhusiano
- mabadilisho ya ajira yako, mapato, na rasilimali.

Ikiwa akaunti yako mtandaoni ya Centrelink inaunganishwa na myGov, unaweza kutuambia mtandaoni kuhusu mabadilisho ya hali yako.

Unaweza pia kutuambia kwa kutumia ama:

- app ya simu ya Express Plus Centrelink
- simu ya kujihudumia ya Centrelink.

Kwa habari zaidi

- nenda kwa servicesaustralia.gov.au/youthallowancejobseeker kupata habari zaidi katika Kiingereza
- nenda kwa servicesaustralia.gov.au/yourlanguage ambapo unaweza kusoma au kusikiliza habari katika lugha yako
- piga simu kwa **131 202** kuongea nasi katika lugha yako kuhusu malipo na huduma ya Centrelink

- Piga simu kwa **132 011** kwa Medicare na **131 272** kwa Child Support. Tujulishe ikiwa unahitaji mkalimani, na tutapanga mmoja kwa bure
- tembelea kituo cha huduma.

Kumbuka: simu kutoka simu yako ya nyumbani kwenda nambari za simu za '13' kutoka popote nchini Australia zinatozwa kwa kiwango kamili. Kiwango hicho kinaweza kutofautiana kutoka bei ya simu ya mtaa na kinaweza pia kutofautiana na watoa huduma wa simu. Simu kwa nambari za simu za '1800' kutoka simu yako ya nyumbani ni bila malipo. Simu kutoka simu za umma na za mkononi zinaweza kupimwa kwa muda na kutozwa kwa kiwango cha juu zaidi.

Kanusho

Maelezo yaliyomo katika chapisho hili yanakusudiwa kama mwongozo pekee wa malipo na huduma. Ni wajibu wako kuamua kama ungependa kuomba malipo na kufanya maombi kuhusiana na hali yako mahususi.



Youth Allowance for job seekers

Youth Allowance for job seekers gives you financial help if you are 21 years of age or younger and looking for work, or temporarily unable to work.

Eligibility for Youth Allowance for job seekers

The rules you need to meet to get Youth Allowance for job seekers depend on your situation.

You must be between 16 and 21 years of age and meet both:

- residence rules
- the income test.

You also need to be one of the following:

- unemployed and looking for work
- sick or injured and unable to do your usual work or study for a short time.

You may not be eligible if you get certain payments from the Department of Veterans' Affairs (DVA).

Your current circumstances will be considered to assess your eligibility for Youth Allowance.

Payment rates for Youth Allowance for job seekers

The amount you can get may change depending on your personal situation. This includes:

- if you have a partner
- if you have children
- if you live at your parent's house
- if you live away from your parent's house to study, train or look for work
- if you own any assets, for example real estate, shares or managed investments
- how much income you and your partner earned in the past 14 days.

If you earn income over a certain amount, it may affect how much you can get.

How to claim Youth Allowance for job seekers

You can claim Youth Allowance for job seekers online using your Centrelink online account through myGov. If you do not have a myGov account or a Centrelink online account, you need to set them up.

If you need help to set up your online account, you can talk to our staff. Let us know if you need an interpreter and we will arrange one for free.

You can start your claim up to 13 weeks before your circumstances will change.

It may be for one of the following reasons:

- you are stopping fulltime studies
- you will be working less hours and you meet the personal income test
- you know you are going to lose your job.

You can withdraw your claim at any time if your financial situation changes.

When you get your first payment

You will need to complete your initial tasks and report your income before we can make your first payment.

In most cases, you will get your first Youth Allowance payment around 2 weeks after we approve your claim. You may have to wait longer if any waiting periods apply. Once your payment starts, we will pay you every 2 weeks.

We will tell you if you have a waiting period and how long you will need to wait. You will also need to report your and your partner's income every 2 weeks.

We calculate the waiting periods that apply to you when we assess your claim. You can expect to hear from us within 21 days of submitting your claim.

The time it takes us to assess your claim does not affect your waiting period.

Change of circumstances

You need to tell us about any changes of circumstances within 14 days. This includes changes for you:

- parents or guardians
- partner
- dependent children.

The changes may include:

- your personal and contact details
- study changes
- your living situation
- name changes
- family situation
- your relationship status
- your employment, income, and asset changes.

If your Centrelink online account is linked to myGov, you can tell us online about changes to your circumstances.

You can also tell us using either:

- the Express Plus Centrelink mobile app
- Centrelink phone self-service.

For more information

- go to servicessaustralia.gov.au/youthallowancejobseeker for more information in English
- go to servicessaustralia.gov.au/yourlanguage where you can read or listen to information in your language
- call **131 202** to speak with us in your language about Centrelink payments and services

- call **132 011** for Medicare and **131 272** for Child Support. Let us know if you need an interpreter, and we will arrange one for free
- visit a service centre.

Note: calls from your home phone to '13' numbers from anywhere in Australia are charged at a fixed rate. That rate may vary from the price of a local call and may also vary between telephone service providers. Calls to '1800' numbers from your home phone are free. Calls from public and mobile phones may be timed and charged at a higher rate.

Disclaimer

The information contained in this publication is intended only as a guide to payments and services. It is your responsibility to decide if you wish to apply for a payment and to make an application with regard to your particular circumstances.